**SERIKALI YA MAPINDUZI ZANZIBAR**

# OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI

# MPANGO KAZI WA KUIMARISHA TAKWIMU ZA JINSIA ZANZIBAR

## 2020-2023

## Septemba, 2020

## 1. Utangulizi

Mahitaji ya kuimarisha takwimu za jinsia yametokana na Mkakati wa Kupunguza Umaskini Zanzibar (MKUZA III) na kutokana na makubaliano ya Ajenda ya 2030 ya Malengo ya Maendeleo Endelevu ili kuhakikisha kuwa 'Hakuna Mtu Anaeachwa Nyuma'. Ili kufikia makubaliano haya, takwimu zinazotumika kupima maendeleo zinapaswa kugawanywa/kuchambuliwa sio kijinsia tu, lakini pia kwa umri, maeneo, elimu, ajira, hali ya ulemavu, pamoja na makundi hatarishi.

Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali (OCGS) imefanya jitihada mbalimbali

za kuimarisha uzalishaji, upatikanaji na matumizi ya takwimu za jinsia ili kufikia malengo hayo. Uimarishaji ulianza kwa kuanzisha kitengo cha takwimu za jinsia ambacho kina jukumu/lengo la kukusanya, kuweka pamoja na kuchambua takwimu za jinsia na kuhakikisha kinajaza mapungufuya takwimu zinazokosekana; kuboresha upatikanaji wa viashiria vya jinsia kwa uchanganuo wa kina vinavyotokana na tafiti, sensa na taarifa za utawala; na kutoa muongozo kwa watoaji wa taarifa juu ya ukusanyaji, uandishi wa ripoti na usambazaji wa takwimu za jinsia.

Licha ya juhudi zote zilizochukuliwa na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali

na mipango/hatua madhubuti za uingizaji wa takwimu za jinsia katika mipango ya maendeleo, bado kuna changamoto kadhaa ambazo zinahitaji kushughulikiwa kwa juhudi za pamoja na wadau mbalimbali. Changamoto hizo ni pamoja na uwezo mdogo wa sekta katika uzalishaji na kusimamia takwimu za jinsia. Hii inapelekea sekta kuwa na utendaji mdogo, takwimu zisizokidhi viwango, ugumu wa kupata takwimu kwa wakati na kupata takwimu zisizojitosheleza katika migawanyo/michanganuo ya makundi mbalimbali. Changamoto nyingine ni ushirikiano na muingiliano mdogo kwa wadau wa takwimu, unachangia ugumu wa kupata taarifa kutoka sekta binafsi

na za Serikali; Aidha, uwasilishaji mdogo, upatikanaji na matumizi madogo ya takwimu za jinsia yanasababisha ugumu katika kutathmini utekelezaji wa mipango ya maendeleo.

Kwa kuwa jinsia ni suala mtambuka, mpango huu wa utekelezaji utasaidia kufuatilia maendeleo na uimarishaji wa ukusanyaji wa takwimu za jinsia katika maeneo matatu ambayo ni; takwimu za matukio ya kijamii, uhamiaji na uhalifu.

## 2. Nini kifanyike katika kuimarisha upatikanaji wa takwimu za jinsia?

Takwimu za jinsia ni mahitaji ya awali katika mipango na kufanya maamuzi yanayolenga kuimarisha na kutoa huduma kwa wanawake na wanaume,

wavulana na wasichana. Ili kutoa na kuimarisha takwimu za jinsia, Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali inahitaji kufanya kazi kwa karibu sana na wazalishaji wa taarifa. Kwa hivyo, Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali imepanga kufanya yafuatayo:

1. Kufanya mikutano ya kila robo mwaka na wadau kupitia Kamati ya Ufundi ya Jinsia ambayo imeundwa na Wakurugenzi wa Sera, Mipango na Utafiti, maafisa wakuu kutoka taasisi nyingine ambao wana majukumu yanayohusiana na wakurugenzi hao, na wenyeviti kutoka taasisi zisizo za Serikali (NGOs).

2. Kutembelea wazalishaji wa data mara kwa mara ili kutathmini maboresho ya kazi zao na kujadili changamoto zozote zinazo kwamisha uzalishaji wa takwimu za jinsia.

3. Kupitia nyenzo za ukusanyaji wa data ikiwemo madodoso yanayotumiwa katika sensa na tafiti kwa lengo la kujumuisha viashiria vya takwimu za jinsia zinazohitajika. Baadhi ya taasisi zina madodoso ambayo hayahusisishi taarifa zinazohitajika kukidhi mahitaji ya ufuatiliaji wa mipango ya maendeleo ya MKUZA au SDG.

4. Kuendesha mafunzo ya kuwajengea uwezo wazalishaji wa takwimu.

5. Kuandaa programu mbalimbali katika vyombo vya habari kwa lengo la kutangaza na kusambaza takwimu za jinsia kupitia wavuti na semina.

## 3. Hali ya sasa ya upatikanaji wa takwimu za kiutawala za matukio ya kijamii, uhamiaji na uhalifu.

***Takwimu za Matukio ya kijamii:*** Kwa muda mrefu, upatikanaji wa takwimu za matukio ya kijamii (Takwimu za Ndoa na Talaka) umekuwa mdogo sana kutokana na changamoto za mfumo uliopo wa ukusanyaji wa takwimu hizo

za kiutawala. Kwa taarifa za ndoa, zinapatikana kupitia fomu zinazojazwa kila linapotekea tukio la kufunga ndoa. Hata hivyo, taarifa za talaka zinaripotiwa kwa nadra (mara chache sana). Kwa taarifa zinazoripotiwa hubakia katika makaratasi na ufanyaji kazi wake huwa ni mdogo, hivyo Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali haiwezi kupata takwimu hizo kwa urahisi.

Viashiria kama kiwango cha ndoa, wastani wa umri katika ndoa ya kwanza na kiwango cha talaka hupatikana katika sensa au tafiti tu ambazo hufanywa kila baada ya miaka mitano hadi kumi. Njia rahisi zaidi ya kupata viashiria hivyo ni kutumia data za kiutawala ambazo

zinatoa takwimu sahihi na kwa wakati uliopo. Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali inakusudia kuimarisha upatikanaji wa takwimu za Ndoa na Talaka kutoka kwenye vyanzo vyote kwa kutumia data za kiutawala.

Kwa sasa hakuna takwimu za kiutawala zinazopatikana hazikidhi mahitaji, ingawa kuna mfumo ambao umetengenezwa kwa ajili ya kusajili taarifa za matukio hayo ya kijamii katika ofisi ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar. Takwimu za kikazi kipya tu ndizo zinazopatikana katika mfumo huu, wakati mifumo mengine haifanyi kazi (kifo, ndoa na talaka). Utaratibu wa kupata takwimu katika mfumo huu uko moja kwa moja

lakini kwa sababu za kiufundi, hakuna muunganisho wa kupata taarifa hizo kwa sasa.

***Takwimu za Uhamiaji:*** Ni muhimu kuimarisha takwimu za uhamaji katika viwango vya Kimataifa na Kikanda. Kwa kufanya hivyo, ipo haja ya kuelewa kwa undani tafsiri halisi za ukusanyaji na uwasilishaji wa takwimu za uhamaji na pia kuelewa vyanzo vikuu vya upatikanani za takwimu za uhamaji. Mahitaji ya kuimarisha data za uhamaji yanatokana na matarajio ya Ajenda ya 2030 kwamba data zinazokusanya zinapaswa kugawanywa kwa hali ya uhamaji.

Upimaji wa kiwango cha wahamaji

unategemea dhana, ufafanuzi, na vigezo mbalimbali, ambavyo mara nyingi ni vigumu kwa nchi kupima. Uwepo wa tafsiri sahihi zitatumika katika kulinganisha takwimu za uhamaji kimataifa. Dhumuni la kuhamia au kuingia nchini ni kiashiria muhimu katika kufahamu takwimu za uhamaji wa kimataifa.

Hivyo, kupima viashiria vya uhamaji, taarifa zilizochanganuliwa kijinsia zinahitajika ili kuondoa changamoto, kuongeza usahihi wa data na kutoa uelewa juu ya vipimo vya uhamiaji. Kwa kuondosha unyanyasaji wa kijinsia katika michakato ya uhamiaji, data zilizochanganuliwa kijinsia ni lazima zikusanywe katika maeneo yote ya

uchambuzi.

Kwa sasa, hakuna takwimu za kiutawala zinazopatikana, hivyo tunategemea taarifa za sensa na tafiti. Hata hivyo, Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali hivi karibuni imeanzisha kitengo cha takwimu za uhamaji, ambapo watendaji wapo katika hatua za awali za kukusanya takwimu za kiutawala kutoka vyanzo tofauti. Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali itatoa takwimu zinazopatikana na zinazokubalika kutoka vyanzo tofauti. Taarifa zote za tafiti zitalinganishwa Kimataifa.

***Takwimu za Uhalifu:*** Takwimu hizi kwa kiasi kikubwa zinazalishwa kutoka

vyanzo tafauti ikiwemo takwimu za kiutawala, tafiti na mara chache kupitia uchunguzi wa matukio.

Kwa Zanzibar, ukusanyaji wa takwimu rasmi za uhalifu unasimamiwa na taasisi zinazosimamia makosa ya jinai kama vile Polisi, Chuo cha Mafunzo, na Mahakama.

Hivyo, Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali inapata takwimu chache zinazokusanywa na taasisi hizo. Takwimu rasmi za uhalifu zinazokusanywa zina vikwazo vingi na vinavyoleta mjadala kutokana na sababu nyingi ikiwemo kuwa hakuna sehemu moja ambayo ndio chanzo kikuu cha kujadili takwimu zote za uhalifu. Aidha,

hakuna makubaliano juu ya namna ya kukusanya takwimu za uhalifu.

Kutokana na uhalisia na ugumu wa matukio ya uhalifu yanavyotokea, mapungufu ya upatikanaji wa takwimu za uhalifu unachangiwa na mambo yafuatayo: - hakuna tafsiri ya wazi ya maneno ya kihalifu; ukosefu wa mifumo na zana za kisasa kuanzia ukusanyaji mpaka uchambuzi wa data; hakuna mfumo wa kuthibitisha data zinazozalishwa; hakuna kituo kimoja cha kuripoti matukio ya uhalifu; na uelewa mdogo wa wafanyakazi wanaoshughulikia takwimu za uhalifu.

Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali inahitaji kuimarisha takwimu rasmi za

uhalifu ambazo zitakidhi viwango vilivyothibitishwa kwa kuwajengea uwezo wafanyakazi, watoa taarifa na wanaokusanya data. Hii itaongeza upatikanaji wa takwimu za uhalifu zilizo katika mgawanyo tafauti na zitakazokidhi viwango vya kimataifa, kikanda na kitaifa.

Kwa sasa, OCGS inaweka takwimu za kesi za uhalifu kwa jinsi, waathiriwa na watuhumiwa kwa jinsi; Ajali na makosa ya barabarani kwa jinsi; makosa dhidi ya mali kwa jinsi; makosa dhidi ya watuhumiwa madawa ya kulevya kwa jinsi; makosa dhidi ya udhalilishaji kijinsia kwa jinsi; malalamiko dhidi ya udhalilishaji kwa aina ya udhalilishaji na jinsi; unyanyasaji wa kijinsia dhidi

ya wanawake na watoto.

## 4. Wajibu wa Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali

Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali imeweka mikakati ya kuimarisha uzalishaji wa takwimu za kijinsia. Kwa kushirikiana na IDC, Ofisi imejipanga kutekeleza malengo ya ajenda 2030 ambayo yanahimiza hakuna kuacha mtu nyuma (lazima kila mtu ahesabiwe) na kutekeleza mahitaji ya MKUZA. Ili kukamilisha lengo hili Ofisi inahitaji msaada (wa kiufundi na kifedha) katika kutekeleza shughuli zote zilizopangwa.

Takwimu za jinsia ni zaidi ya data zilizo katika mgawanyo wa jinsi. Ofisi ya

Mtakwimu Mkuu wa Serikali, kama mtoaji wa takwimu rasmi, itahakikisha kuwa data zote zinazokusanywa kutoka vyanzo vyote zinawasilishwa kwa jinsi na mgawanyo wa umri, maeneo, elimu, ajira, hali ya ulemavu na makundi hatarishi.

## 5. Mpango

Lengo kuu la kuimarisha takwimu za jinsia ni kuongeza matumizi ya takwimu za jinsia kwa kuzalisha takwimu zilizobora, zinazoaminika, zinazoweza kupatikana kwa wakati ili kuziwasilisha katika utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya kitaifa, kikanda na kimataifa. Matokeo ya mpango huu yanatarajiwa kuboresha uzalishaji na

upatikanaji wa data za jinsia kwa urahisi. Mpango huu utafanyiwa marekebisho kila mwaka.

| **Kanuni ya Kwanza** - Data zijumuishe makundi ya watu wote | | | |
|---|---|---|---|
| Namba ya Mpango | Kazi iliyopangwa | Muda wa Utekelezaji | Hali ya muda (Mrefu-MR, Kati-MK, Mfupi-MF) |
| **1.1** | Kuangalia data zilizokosekana kwa kutumia ripoti za uchambuzi wa tafiti nyingine zilizofanyika. | 2020-2023 | MK |
| **1.2** | Kutathmini uwezo wa sekta katika uzalishaji na usimamizi wa data. | 2020, robo ya 4 | MF |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | OCGS itatathmini mfumo wa sasa wa ukusanyaji wa data ili kuona utaratibu unaotumika kupata taarifa, namna zinavyokusanywa, vyanzo vipi vya taarifa, ubora wa taarifa, n.k.<br>*Tathmini hii itafanywa kwa kutumia dodoso fupi litakalotayarishwa na OCGS, kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo ili kupata taarifa za uwezo wa sekta.* | | |

| **Kanuni ya Pili** - Takwimu zote, kila inapowezekana zinapaswa kuwekwa katika mchanganuo tafauti ili kupata taarifa sahihi za watu wote. | | | |
|---|---|---|---|
| Namba ya | Kazi iliyopangwa | Muda wa Utekelezaji | Hali ya muda |
| 2.1 | Kusaidia wazalishaji wa data katika kuzalisha data zilizogawanywa kwa umri, jinsia, maeneo,ulemavu, hali ya uhamiaji, hali ya uchumi, n.k. Hii itatekelezwa kwa kuzifanya ziara | 2021-robo ya 1 | MR |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | *sekta kila mwaka na kujadili ukusanyaji wa data, changamoto zilizopo za data n.k.* | | |
| 2.2 | Kutumia data za kiutawala zilizopo ili kuziripoti kwa ajili ya utekelezaji wa mpango wa kitaifa (MKUZA), Mkataba wa Umoja wa Afrika (Agenda 2063) na Mpango Endeleve wa Maendeleo wa kimataifa (SDGs). | 2020-2023 | MR |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 2.3 | Kuanzisha metadata kwa viashiria vya jinsia visivyo na metadata vya Malengo Endelevu ya Maendeleo (SDGs), kuandaa utaratib maalumu wa kukusanya, kuhariri na kuchakata data kwa vyanzo vyote vinavyozalisha data.<br>*OCGS itahitaji msaada kutekeleza kazi hii (kiufundi na kifedha).* | 2020-2023 | MR |

| **Kanuni ya Tatu -** Takwimu inapaswakukusanywa kutoka kwa vyanzo vyote vinavyopatikana. | | | |
|---|---|---|---|
| Namba | Kazi iliyopangwa | Muda wa Utekelezaji | Hali ya muda |
| 3.1 | Kushirikiana na wadau ili kutafuta vyanzo vipya vya data na kutayarisha njia za kujaza mapengo kwa viashiria vilivyokosa data.<br>*Hii itafanywa kupitia vikao vya Kamati ya wataalamu.* | 2021, robo ya 1- robo ya 4 | MR |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 3.2 | Kupitia viashiria vya jinsia vya SDGs ambavyo vinapatikana kwenye sensa na tafiti (kazi endelevu ambayo tayari imeanza). | 2020-2023 | MR |
| **Kanuni ya Nne –** Wanaohusika na ukusanyaji wa data na uzalishaji wa takwimu ni lazima wawajibike. | | | |
| Namba | Kazi iliyopangwa | Muda wa Utekelezaji | Hali ya muda |
| **4.1** | Kuandaa Mikataba ya makubaliano kati ya watumiaji na wazalishaji wa takwimu za jinsia. Hivi sasa, kuna ushirikiano mdogo kati ya sekta. | 2021, robo ya 2 | MF |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | OCGS inahitaji kuwa na ushirikiano mzuri kati ya sekta ili kuimarisha ushiriki wa sekta katika maendeleo ya takwimu. | | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **4.2** | *OCGS inahitaji msaada wa* Kufafanua taratibu za kudhibiti ubora/vipimo vya ubora ambavyo vinaweza kutumiwa na asasi za kiraia katika kuzalisha takwimu rasmi na zilizo bora za jinsia.<br><br>*OCGS itahitaji msaada wa kiufundi kuandaa na kutekeleza* | 2021-2023 | MR |
| **Kanuni ya Tano** - Uwezo wa kiufundi na rasilimali watu wa kukusanya, kuchambua, na kutumia data zilizogawanywa ni lazima uimarishwe, kwa kuweka mipango imara na endelevu ya kifedha. | | | |
| Namba | Kazi iliyopangwa | Muda wa | Hali ya |

| | | Utekelezaji | muda |
|---|---|---|---|
| 5.1 | Kuwajengea uwezo wanaokusanya, wanaotunza na wanaochambua data ili kuzijumuisha data wanazozalisha katika mgawanyo tafauti. | 2021, robo ya 4 | MF |
| 5.2 | Kufanya kazi kwa kushirikiana na wazalishaji wa data ili kuboresha nyenzo za kukusanya data.<br><br>*Hii itafanywa kupitia mikutano ya Kamati ya wataalamu.* | 2021, robo ya 1- robo ya 4 | MR |
| 5.3 | Kuzipitia data zilizopo na | 2021 - 2023 | MR |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | kushajiisha wazalishaji wa data kuziweka data hizo kwenye mfumo wa kielektronik kutoka mfumo wa makaratasi.<br><br>Lengo la kazi hii ni kuhamisha taarifa muhimu kutoka kwenye fomu za ndoa na talaka. Hivi sasa taarifa hukusanywa wakati wa tukio la ndoa kupitia fomu, na taarifa hizi hubakia kwenye karatasi. Kwa kurahisisha upatikanaji wa taarifa hizo, taasisi | | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | inayohusika ni vyema kuhamisha data kwenye mfumo wa elektroniki. Sio lazima katika mfumo wa kiprogramu hata katika mfumo rahisi wa kieletroniki. *OCGS inahitaji msaada (wa kiufundi na kifedha).* | | |
| **6. Masuala Mtambuka** | | | |
| Namba | Kazi iliyopangwa | Muda wa Utekelezaji | Hali ya muda |
| 6.1 | Kutayarisha vipeperushi ambavyo vitaonyesha viashiria muhimu vya jisia. | 2021, Robo ya 2 | MT |